


EPISCOPAL CHURCH of the  
**HEAVENLY REST**

God's Love. For All.

---

Jumapili ya Kwanza baada ya Krismasi  
Sala ya Asubuhi  
Jumapili, Desemba 28, 2025  
Saa 1:00 jioni



First Sunday after Christmas  
Morning Prayer in Swahili  
Sunday, December 28, 2025  
1:00 in the afternoon

## SHAIRI LA SIKU

I Yohana 4:9

Mapendo ya Mungu yameonekana kwetu: alimutuma Mwana wake wa pekee katika dunia kusudi tupate uzima wa milele.

## WIMBO WA KUINGILIA

*Wote kusimama*

## WITO WA KUABUDU

Tumekusanyika pamoja kama jamaa ya Mungu mbele ya Baba yetu, tukivutwa na Roho yake, kusifu Jina lake, kusikia na kupokea Neno lake takatifu. kumwomba usamehe kwa zambi zetu, kuombea mahitaji yetu na ya dunia, kufurahi katika mapendo yake, na kutumwa katika salama yake.

## MWALIKO

Ee Bwana, ufungue midomo yetu.

**Na kinywa chetu kitaonyesha sifa yako.**

Matendo ya Bwana ni makubwa na ya ajabu!

**Wakati tulikuwa tungali katika giza, alisikia kilio chetu.**

Mapendo ya Mungu yameonekana kwetu.

**Alituma Mwana wake, ili tupate uzima wa milele.**

*Wimbo wa Biblia au wimbo mwingine.*

## WIMBO

## KUUNGAMA DHAMBI

*Muhudumu aseme:*

Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu.

Tukikiri zambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, hata atatuondolea zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote.

I Yoane 1:8-9

*Muhudumu aseme:*

Tukiri zambi zetu kwa Mungu Mwenyezi.

*Wote wapige magoti na kusema*

**Mungu Mwenyezi, Baba yetu ya mbinguni, tumekosea wewe, na tumekosea jirani zetu, kwa mawazo yetu, na kwa maneno yetu, na kwa matendo yetu, na kwa maovu tuliyoyatenda, na kwa mema tusiyoyatenda, kosa letu wenyewe. Sisi tunatubu kabisa. Kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo, utusamehe yote yaliyopita; utuwezeshe tangu leo kukutumikia, katika upya wa uzima. Kwa utukufu wa Jina lako. Amina.**

*Muhudumu au mutu mwingine asiye Kasisi, akipiga magoti atumie ombi hili.*

Ee Mungu, mwenye rehema, tunakusihi, utupe sisi, watu wako waaminifu, usamehe na salama, ili tusafishwe zambi zetu zote, na tukutumikie na nia tulivu; kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

**Amina.**

*Zaburi ya Siku isomwe au iimbwe.*

## ZABURI 148

1 Haleluya. Msifuni BWANA kutoka mbinguni; Msifuni katika mahali palipo juu.

2 Msifuni, enyi malaika wake wote; Msifuni, majeshi yake yote.

3 Msifuni, jua na mwezi; Msifuni, nyota zote zenye mwanga.

4 Msifuni, enyi mbingu za mbingu, Nanyi maji mlioko juu ya mbingu.

5 Na vilisifu jina la BWANA, Kwa maana aliamuru, vikaumbwa.

6 Amevithibitisha hata milele na milele, Ametoa amri wala haitapita.

7 Msifuni BWANA kutoka nchi, Enyi nyangumi na vilindi vyote.

8 Moto na mvua ya mawe, theluji na mvuke, Upepo wa dhoruba utimizao neno lake.

9 Milima na vilima vyote, Miti yenye matunda na mierezi yote.

## OPENING SENTENCE

1 John 4:9

God's love was manifested in us: He sent His only Son into the world so that we might have eternal life.

## PROCESSIONAL HYMN

*Stand for the Procession*

## CALL TO WORSHIP

We are gathered together as God's family before our Father, drawn by his Spirit, to praise his Name, to hear and receive his holy Word. to ask him to forgive us for our sins, to pray for our needs and the needs of the world, to rejoice in his love, and to be sent to his safety.

## INVITATORY

O Lord, open our lips.

**And our mouth shall proclaim your praise.**

Great and marvelous are the works of the Lord!

**While we were still in darkness, he heard our cry.**

God's love has been revealed to us.

**He sent his Son, so that we might have eternal life.**

*A song from the Bible or another song is sung.*

## HYMN

## CONFESSION OF SIN

*The Minister should say:*

If we say that we have no sin, we deceive ourselves, and the truth is not in us. If we confess our sins, he who is faithful and just will forgive us our sins and cleanse us from all unrighteousness.

1 John 1:8-9

*The Minister should say:*

Let us confess our sins to God Almighty.

*All should kneel and say:*

**Almighty God, our heavenly Father, we have sinned against you and against our neighbors, in thought and word and deed, in the evil we have done and in the good we have not done, through our own deliberate fault. We are truly sorry, and repent of all our sins. For the sake of your Son Jesus Christ, who died for us, forgive us all that is past; and grant that we may serve you in newness of life to the glory of your name. Amen.**

*A minister or other person who is not a priest, kneeling should use this request:*

Grant, we ask you, merciful Lord, to your faithful people pardon and peace, that they may be cleansed from all their sins, and serve you with a quiet mind, through Jesus Christ our Lord.  
**Amen.**

*The Psalm of the Day should be read or sung.*

## PSALM 148

1 Praise the Lord! Praise the Lord from the heavens; praise him in the heights!

2 Praise him, all his angels; praise him, all his host!

3 Praise him, sun and moon; praise him, all you shining stars!

4 Praise him, you highest heavens and you waters above the heavens!

5 Let them praise the name of the Lord, for he commanded and they were created.

6 He established them forever and ever; he fixed their bounds, which cannot be passed.

7 Praise the Lord from the earth, you sea monsters and all deeps,

8 fire and hail, snow and frost, stormy wind fulfilling his command!

9 Mountains and all hills, fruit trees and all cedars!

IO Hayawani, na wanyama wafugwao, Vitambaavyo, na ndege wenye mbawa.  
II Wafalme wa dunia, na watu wote, Wakuu, na watawala wote wa dunia.  
12 Vijana wa kiume, na wanawali, Wazee, na watoto;  
13 Na walisifu jina la BWANA, Maana jina lake peke yake limetukuka; Adhama yake i juu ya nchi na mbingu.  
14 Naye amewainulia watu wake pembe, Sifa za watauwa wake wote; Wana wa Israeli, watu walio karibu naye. Haleluya.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu:  
**kama ulivyokuwa mwanzo ulivyo sasa, hata milele na milele. Amina.**

WIMBO

*Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO LA KALE kisomwe.*

SOMO LA KWANZA

Isaya 63:7-9

*Musomaji aseme kwanza:*

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Kitabu cha Isaya.

Nitautaja wema wa Bwana, sifa za Bwana kwa yote aliyotukirimia Bwana; na wingi wa wema wake kwa nyumba ya Israeli, aliowakirimia kwa rehema zake, na kwa wingi wa wema wake. Maana alisema, Hakika ndio watu wangu hawa, wana wasio na hila; akawa Mwokozi wao. Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale.

Hilo ndilo Neno la Bwana.  
**Asante kwa Mungu.**

WIMBO

*Kuketi. Kipande kinachotoka AGANO JIPIYA kisomwe.*

SOMO LA PILI

Waebrania 2:10-18

*Musomaji aseme kwanza:*

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Barua kwa Waebrania.

Kwa kuwa ilimpasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wana wengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; akisema, Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; Katikati ya kanisa nitakuambia sifa. Na tena, Nitakuwa nimemtumaini yeye. Na tena, Tazama, mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu. Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa. Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake. Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.

Hilo ndilo Neno la Bwana.  
**Asante kwa Mungu.**

WIMBO

10 Wild animals and all cattle, creeping things and flying birds!  
11 Kings of the earth and all peoples, princes and all rulers of the earth!  
12 Young men and women alike, old and young together!  
13 Let them praise the name of the Lord, for his name alone is exalted; his glory is above earth and heaven.  
14 He has raised up a horn for his people, praise for all his faithful, for the people of Israel who are close to him. Praise the Lord!

Glory be to the Father, and to the Son, and to the Holy Spirit:  
**As it was in the beginning, is now, and ever shall be, world without end. Amen.**

#### HYMN

*All Sit. A passage from the OLD TESTAMENT should be read.*

#### FIRST READING

Isaiah 63:7-9

*Let the reader say first:*

Hear the Word of the Lord as written in the Book of Isaiah.

I will recount the gracious deeds of the Lord, the praiseworthy acts of the Lord, because of all that the Lord has done for us, and the great favour to the house of Israel that he has shown them according to his mercy, according to the abundance of his steadfast love. For he said, 'Surely they are my people, children who will not deal falsely'; and he became their saviour in all their distress. It was no messenger or angel but his presence that saved them; in his love and in his pity he redeemed them; he lifted them up and carried them all the days of old.

The Word of the Lord.  
**Thanks be to God.**

#### HYMN

*All Sit. A passage from the NEW TESTAMENT should be read.*

#### SECOND READING

Hebrews 2:10-18

*Let the reader say first:*

Hear the Word of the Lord as written in the Book of Hebrews.

It was fitting that God, for whom and through whom all things exist, in bringing many children to glory, should make the pioneer of their salvation perfect through sufferings. For the one who sanctifies and those who are sanctified all have one Father. For this reason Jesus is not ashamed to call them brothers and sisters, saying, 'I will proclaim your name to my brothers and sisters, in the midst of the congregation I will praise you.' And again, 'I will put my trust in him.' And again, 'Here am I and the children whom God has given me.' Since, therefore, the children share flesh and blood, he himself likewise shared the same things, so that through death he might destroy the one who has the power of death, that is, the devil, and free those who all their lives were held in slavery by the fear of death. For it is clear that he did not come to help angels, but the descendants of Abraham. Therefore he had to become like his brothers and sisters in every respect, so that he might be a merciful and faithful high priest in the service of God, to make a sacrifice of atonement for the sins of the people. Because he himself was tested by what he suffered, he is able to help those who are being tested.

The Word of the Lord.  
**Thanks be to God.**

#### HYMN



*Musomaji aseme kwanza:*

Sikieni Neno la Bwana kama lilivyoandikwa katika Injili ya Matayo.

Na hao walipokwisha kwenda zao, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto, kasema, Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize. Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda zake Misri; akakaa huko hata alipokufa Herode; ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema, Kutoka Misri nalimwita mwanangu. Ndipo Herode, alipoona ya kuwa amedhihakiwa na wale mamajusi, alighadhabika sana, akatuma watu akawaua watoto wote wanaume waliokuwako huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenye miaka miwili na waliopungua, kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale mamajusi. Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na nabii Yereimia, akisema, Sauti ilisikiwa Rama, Kilio, na maombolezo mengi, Raheli akiwalilia watoto wake, Asikubali kufarijiwa, kwa kuwa hawako. Hata alipofariki Herode, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri, akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto. Akaondoka akamchukua mtoto na mamaye, akafika nchi ya Israeli. Lakini aliposikia ya kwamba Arkelao anamiliki huko Uyahudi mahali pa Herode babaye, aliogopa kwenda huko; naye akiisha kuonywa katika ndoto, akasafiri pande za Galilaya, akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazorayo.

Hilo ndilo Neno la Bwana.  
Asante kwa Mungu.

## WIMBO WA INJILI

### KUHUBIRI

Bikole Mulanda, *Waziri wa Usharika wa Kiswahili*

### IMANI YA MITUME

*Watu wasimame kuhakikisha IMANI YA MITUME*

**Ninamwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia; Na Yesu Kristo, Mwana wake wa pekee, Bwana wetu, aliyetwaa mwili kwa tendo la Roho Mutakatifu, akazaliwa na Bikira Maria. Akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimuni mwa wafu, akafufuka katika wafu siku ya tatu, akapanda mbinguni, anakaa kwa mukono wa kuume wa Mungu, Baba Mwenyezi, ndipo atakuja tena kuhukumu wazima na wafu. Ninamwamini Roho Mutakatifu, Kanisa katolika takatifu, ushirika wa watakatifu, on-doleo la zambi, ufufuko wa mwili, na uzima wa milele. Amina.**

### MAOMBI

*Kupiga magoti*

Bwana utuhurumie.  
**Kristo utuhurumie.**  
Bwana utuhurumie.

### SALA YA BWANA

*Wote*

**Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, duniani kama mbinguni. Utupe leo chakula chetu cha kila siku; utusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe waliotukosea. Usitulete katika majaribu, lakini utuokoe katika uovu. Kwani kwako ufalme, uwezo na utukufu, milele na milele, Amina.**

*Let the reader say first:*

Hear the Word of the Lord as written in the Gospel of St. Matthew.

Now after they had left, an angel of the Lord appeared to Joseph in a dream and said, 'Get up, take the child and his mother, and flee to Egypt, and remain there until I tell you; for Herod is about to search for the child, to destroy him.' Then Joseph got up, took the child and his mother by night, and went to Egypt, and remained there until the death of Herod. This was to fulfil what had been spoken by the Lord through the prophet, 'Out of Egypt I have called my son.' When Herod saw that he had been tricked by the wise men, he was infuriated, and he sent and killed all the children in and around Bethlehem who were two years old or under, according to the time that he had learned from the wise men. Then was fulfilled what had been spoken through the prophet Jeremiah: 'A voice was heard in Ramah, wailing and loud lamentation, Rachel weeping for her children; she refused to be consoled, because they are no more.' When Herod died, an angel of the Lord suddenly appeared in a dream to Joseph in Egypt and said, 'Get up, take the child and his mother, and go to the land of Israel, for those who were seeking the child's life are dead.' Then Joseph got up, took the child and his mother, and went to the land of Israel. But when he heard that Archelaus was ruling over Judea in place of his father Herod, he was afraid to go there. And after being warned in a dream, he went away to the district of Galilee. There he made his home in a town called Nazareth, so that what had been spoken through the prophets might be fulfilled, 'He will be called a Nazorean.'

The Word of the Lord.

**Thanks be to God.**

## HYMN OF THE GOSPEL

## SERMON

Bikole Mulanda, *Swahili Minister*

## THE APOSTLES' CREED

*All People should stand and say the APOSTLES' CREED:*

**I believe in God, the Father almighty, creator of heaven and earth; I believe in Jesus Christ, his only Son, our Lord. He was conceived by the power of the Holy Spirit and born of the Virgin Mary. He suffered under Pontius Pilate, was crucified, died, and was buried. He descended to the dead. On the third day he rose again. He ascended into heaven, and is seated at the right hand of the Father. He will come again to judge the living and the dead. I believe in the Holy Spirit, the holy catholic Church, the communion of saints, the forgiveness of sins the resurrection of the body, and the life everlasting. Amen.**

## THE PRAYERS

*All that are able to should kneel:*

Lord, have mercy upon us.

**Christ, have mercy upon us.**

Lord, have mercy upon us.

## THE LORD'S PRAYER

*All pray.*

**Our Father in heaven, hallowed be your Name, your kingdom come, your will be done, on earth as in heaven. Give us today our daily bread. Forgive us our sins as we forgive those who sin against us. Save us from the time of trial, and deliver us from evil. For the kingdom, the power, and the glory are yours, now and for ever. Amen.**

Ee Bwana utuonyeshe rehema yako;  
**Utupe sisi wokovu wako.**  
Ee Bwana uwabariki watawala wetu;  
**Utusikie kwa rehema yako tukikuomba.**  
Uwavike haki wahudumu wako;  
**Uwafurahishe wachaguliwa wako.**  
Ee Bwana uwaokoe watu wako;  
**Uubariki uriti wako.**  
Ee Bwana utupe salama kwa siku zetu;  
**Na utukufu wako uwe popote duniani.**  
Ee Mungu, utusafishe mioyo yetu;  
**Na ututegemeze na Roho yako Mutakatifu.**

#### SALA YA SIKU

Mungu Mwenyezi, uliyefanya ajabu kutuumba kwa sura yako mwenyewe, na ajabu kubwa zaidi kutuokoa kwa Mwana wako; utupe sisi kwamba, kama alivyokuja kugawanya nasi asili yetu ya mwili, vivyo hivyo tugawanye naye uzima wa uungu wake, anayeishi na kutawala na wewe na Roho Mutakatifu, Mungu mumoja, sasa hata milele. **Amina.**

#### SALA KWA SALAMA

Baba Mungu, uliye mkuu wa salama na mupenda wa upatano, kukujua wewe ni uzima wa milele, kukutumikia wewe ni uhuru wa kweli. Utulinde sisi watumishi wako katika mashambulio yote ya adui zetu; ili sisi tukitumainia ulinzi wako, tusiogope nguvu ya adui wote; kwa uwezo wa Yesu Kristo, Bwana wetu. **Amina.**

#### SALA KWA NEEMA

*Muhudumu na watu wanaweza kusema pamoja.*

Ee Bwana, Baba yetu ya mbinguni, Mungu Mwenyezi unayeishi milele, uliyetusaidia tuione siku hii salama; utulinde leo kwa uwezo wako mkuu, tusianguke katika zambi, wala tusiingie katika hatari yo yote, lakini matendo yetu yote yaongozwe nawe, ili tuyatende siku zote yaliyo ya haki mbele yako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. **Amina.**

#### MAOMBI YA KANISA

Tuombe Kanisa na dunia na tumushukuru Mungu kwa wema wake wote.

*Mwombezi huomba kwa ajili ya mahitaji ya kanisa na ya ulimwengu pasipo kuona.*

*Mwombezi anamaliza sala kwa maneno haya:*

Na tunalisifu jina lako takatifu kwa watumishi wako wote wanaotoka katika uzima huu, wanaokuamini na wanaokuogopa. Tunakusihi utupe neema tufuate desturi zao nzuri, tukutane nao katika ufalme wako wa mbinguni. Utupe sisi hivi, Ee Bwana, kama tunavyoviomba kwa Yesu Kristo Mwana wako, Mwokozi wetu. **Amina.**

*Maombi mengine yanaweza kusemwa.*

#### MATANGAZO NA SADAKA

*Wimbo na kupokea sadaka.*

#### NEEMA

*Watu Wote.*

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mutakatifu, ukae nasi sote, milele na milele. **Amina.**

#### WIMBO YA KUTOKA



Show us your mercy, O Lord;  
**And grant us your salvation.**  
 O Lord, save the State;  
**And mercifully hear us when we call upon you.**  
 Endue your ministers with righteousness;  
**And make you chosen people joyful.**  
 O Lord, save your people;  
**And bless your inheritance.**  
 Give peace in our time, O Lord.  
**May your glory be everywhere in the world .**  
 O God, make clean our hearts within us;  
**And take not your Holy Spirit from us.**

#### THE COLLECT OF THE DAY

Almighty God, who didst wonderfully create us in thine own image, and the greater wonder of saving us by thy Son; grant that, as he came to share with us our fleshly nature, so we may share with him the life of his divinity, who liveth and reigneth with thee and the Holy Spirit, one God, now and for ever. **Amen.**

#### THE COLLECT FOR PEACE

O God, who art the author of peace and lover of concord, in knowledge of whom standeth our eternal life, whose service is perfect freedom: Defend us, thy humble servants, in all assaults of our enemies; that we, surely trusting in thy defense, may not fear the power of any adversaries; through the might of Jesus Christ our Lord. **Amen.**

#### THE COLLECT FOR GRACE

*The Minister and the people say this prayer together.*

**O Lord, our heavenly Father, almighty and everlasting God, who has safely brought us to the beginning of this day; defend us in the same with your mighty power; and grant that this day we fall into no sin, neither run into any kind of danger, but that all our doings may be ordered by your governance, to do always that is righteous in your sight; through Jesus Christ our Lord. Amen.**

#### PRAYERS OF THE CHURCH

Let us pray for the Church and the world and let us thank God for all his goodness.

*The intercessor prays for the needs of the church and the world extemporaneously.*

*The intercessor ends the prayer with these words:*

And we praise your holy name for all your servants who have departed this life, who believe in you and who fear you. We ask you to give us the grace to follow their good example, to meet them in your heavenly kingdom. Grant this, O Lord, as we ask for it from Jesus Christ your Son, our Savior. **Amina.**

*Other prayers may be said.*

#### ANNOUNCEMENTS AND OFFERING

*A song is sung during the offering.*

#### THE GRACE

*All Say*

**The grace of our Lord Jesus Christ, and the love of God, and the fellowship of the Holy Spirit, be with us all evermore. Amen.**

#### RECESSIONAL HYMN





## WAHUDUMU WA LITURUJIA

*Muhubiri/Preacher - Bikole Mulanda, Swahili Minister*

*Kwaya/Choir - Aleluya Kwaya*

*Musomaji/Lay Minister - Bijoux Mashauri*

*Washemasi/Greeters & Ushers - Baya Lushawe, Mkyombwe*



---

602 Meander Street      Phone: (325) 677-2091  
Abilene, Texas 79602      Email: [info@heavenlyrestabilene.org](mailto:info@heavenlyrestabilene.org)  
Website: [heavenlyrestabilene.org](http://heavenlyrestabilene.org)      Social media: [@heavenlyrestabilene](https://www.facebook.com/heavenlyrestabilene)

### CLERGY AND STAFF

The Reverend David F. Romanik, <i>Rector</i>	Carol Ann Weston, <i>Director of Children &amp; Family Ministries</i>
The Reverend Ashley Powers, <i>Associate Rector</i>	Thomas Pavlechko, <i>Organist and Director of Music</i>
The Reverend Amanda Watson, <i>Assistant Rector for Community Life</i>	Elizabeth Knauer, <i>Music Assistant, Choristers</i>
The Reverend Karen Boyd, <i>Assisting Priest</i>	Laura Dickson, <i>Music Assistant, Children's Choir</i>
The Reverend Dr. Doug Thomas, <i>Priest in Residence</i>	Jen Rogers, <i>Director of Communications and Stewardship</i>
The Reverend Dr. Russell Dickerson, <i>Deacon</i>	Lydia Hurt, <i>Parish Manager</i>
The Reverend Joe Biles, <i>Deacon and Pastoral Assistant</i>	Brenda Fisher, <i>Parish Accountant</i>
Bikole Mulanda, <i>Swahili Minister</i>	Robert Becerra, <i>Sexton</i>
Luke Teten, <i>Verger</i>	Dorothy Guerra, <i>Housekeeper</i>
	Anne Jones, <i>Nursery Manager</i>

### VESTRY AND APPOINTED OFFICERS

Kate Haney, *Senior Warden*; Harry Hurt, *Junior Warden*; Sharon Lawler, *Secretary*; David Christianson, Michael Christie, Dru Hall, Diane Stearns, Kimberly Brumley, Jay Hardaway, Norene Mansell, John Nichols, Mary Reyes, Elizabeth Niblo Wallace, *Chancellor*; and Sam Cutbirth, *Treasurer*